TANGAZO LA SERIKALI NA. 662 la tarehe 8/9/2023

SHERIA YA TOZO ZA BARABARA NA MAFUTA,
(SURA YA 220)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

## AMRI YA MSAMAHA WA TOZO YA BARABARA NA MAFUTA KWA MRADI WA UZALISHAJI WA MBOLEA ZA ASILI KWA KAMPUNI YA ITRACOM FERTILIZER YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Tozo ya Barabara na Mafuta kwa Mradi wa Uzalishaji wa Mbolea za Asili kwa Kampuni ya Itracom Fertilizer ya mwaka 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, tozo zote za barabara na mafuta yaliyoanishwa katika Jedwali la Amri hii yaliyoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Kampuni ya Itracom Fertilizer kwa ajili ya mradi wa uzalishaji wa mbolea za asili zinasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na tozo za barabara na mafuta zitapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa mafuta yatatumika kwa matumizi mengine au yatahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafikia ukomo tarehe 26 Juni, 2024 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Itracom Fertilizer na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 05 Aprili, 2022.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| NA. | AINA | KIPIMO | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Dizeli | Lita | 8,400,000 |
| 2. | Petroli | Lita | 20,000 |

Dodoma,
25th August, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*